ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 18 ***1st May, 2020***

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.18. Vol.101 dated 1 May, 2020
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 303 lililotolewa1/5/2020

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA NA. 272)

AMRI

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))

AMRI YA MAMLAKA YA UGAVI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA NAMTUMBO ("NAMTUMBO WSSA") (MAREKEBISHO YA BEI ZA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2020

Kichwa cha Jina

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Namtumbo ("Namtumbo WSSA") (Marekebisho ya Bei za Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira), 2020.

Bei na tozo

2. Bei na tozo za majisafi na usafi wa mazingira za Namtumbo WSSA zinarekebishwa kwa kuzingatia Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo au kabla tarehe 31 Mei, 2020, Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Namtumbo itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili ;

(b) Mamaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(c) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo itawaunganisha wateja wake wote kwa dira za maji ifikapo tarehe 30 Juni, 2020;

(d) ifikapo au kabla tarehe 31 Mei, 2020, Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo iandae mpango wa kuwabaini wateja wasiojiweza waliopo katika eneo lake la huduma na kuwapatia huduma ya maji kwa namna iliyo nafuu;

(e) ifikapo au kabla tarehe 31 Mei, 2020 Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira iandae na kuwasilisha EWURA mpango wa kuwafikia wateja wake kwa lengo la kutoa elimu juu ya Huduma za maji;

(f) ifikapo au kabla tarehe 31 Aprili, 2020, Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Namtumbo iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma kuhusu utekelezaji wa bei mpya, ikiwa ni pamoja na Serikali na wawakilishi wa dini na wa wananchi, katika eneo lake la huduma;

(g) Namtumbo WSSA itanunua na kutunza hifadhi dira za kutosha kwa ajili ya kubadilisha zile zilizokwisha muda wake ili zoezi la ubadilishwaji wa dira lifanyike kwa muda mfupi kadri iwezekanavyo;

(h) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Tatu;

(j) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(k) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo katika siku zijazo.

Kutengua Amri ya Bei Na. 11-014 la 1 Juni, 2011

4. Amri hii inatengua matumizi ya Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo Na. 11-014 katika eneo linalohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo ("Namtumbo WSSA").

_____

JEDWALI LA KWANZA

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Aina ya Mteja	Bei za Sasa	Bei Iliyoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	540	800	895	930
Taasisi	1,000	1,200	1,440	1728
Biashara	1,025	1,230	1,476	1771
Viwanda	-	1,230	1476	1771
Boza	-	1,107	1328	1594
Magati	1,000	1,200	1500	1500

Jedwali Namba 1(b): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/ Mwezi)

Aina ya Mteja	Bei za Sasa	Bei Iliyopendekezwa			Bei Iliyoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22	2019/20 Kabla 31 Desemba 2019	2020/21	2021/22
Majumbani	7,000	12,000	12,000	12,000	7,000	Haijaidhinishwa	
Taasisi	24,500	25,000	25,000	25,000	24,500		
Biashara	24,500	25,000	25,000	25,000	24,500		
Viwanda	-	25,000	25,000	25,000	24,500		
Boza	-	25,000	25,000	25,000	24,500		
Magati	24,500	25,000	25,000	25,000	24,500		

Tangazo la Serikali Na. 303 (linaendelea)

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya sasa	Ada zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	22,500	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na ufundi kama ilivyobainishwa katika Kanuni za Majisafi za mwaka 2013		
Taasisi	51,500			
Biashara	51,500			
Viwanda	-			

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Aina ya Mteja	Ada za sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	4,000	4,000	4,000	4,000
Taasisi	50,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	4,000	6,000	6,000	6,000
Viwanda	-	15,000	15,000	15,000

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(h))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Kazi zitakazofanyika	Kiwango katika Shilingi (million)			Melezo
	2019/20	2020/21	2021/22	
Ukarabati				
Kukarabati Matangi ya Maji ya Namtumbo na Minazini	21.6	5.7	4.0	Ikamilike ifikapo Juni 2022
Kukarabati na kubadilisha tekeo la maji	15	3.0	1.2	Ikamilike ifikapo Juni 2022
Kubadlisha mabomba 2019/20, 10; 2020/21,10; 2021/22,8	20	35	35	Ikamilike ifikapo Juni 2022

Tangazo la Serikali Na. 303 (linaendelea)

Kazi zitakazofanyika	Kiwango katika Shilingi (million)			Melezo
	2019/20	2020/21	2021/22	
Ukarabati				
Jumla ya Ukarabati	56.6	43.7	40.2	
Uwekezaji Mpya				
Kununua mita za maji 531 2019/20, 375 mwaka 2020/21, na 312 mwaka 2021/22	28.83	30.125	32.4	Ikamilike ifikapo Juni 2022
Kununua vitendea kazi	10.14	19.5	23	Ikamilike ifikapo Juni 2022
Jumla Uwekezaji Mpya	38.97	49.625	55.4	
Jumla Uwekezaji wote	95.57	93.325	95.6	

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Kiwango cha idadi ya watu wanaoishi katika eneo lililofikiwa na mtandao wa maji	%	67	69	72
Kiwango katika asilimia cha idadi ya watu wanaohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo	%	58	60	62
Kiwango cha upotevu wa maji (NRW)	%	24	22	20
Wastani wa muda wa utoaji huduma	Saa	16	18	20
Kiwango cha Wateja wa Dira	%	95	100	100
Kiwango cha Ufanisi wa Ukusanyaji mapato	%	75	90	95

Tangazo la Serikali Na. 303 (linaendelea)

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(j))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI ZA KITANZANIA KATIKA MILIONI)

Maelezo	2019/2020	2020/2021	2021/2022
Matengenezo na Uendeshaji			
Uzalishaji	121.38	125.36	129.82
Usambazaji	117.13	131.74	146.57
Majitaka	0.0	0.0	0.0
Matengenezo na Ukarabati	23.5	18.0	13.50
Utumishi	58.25	60.44	65.59
Utawala	61.57	71.16	81.94
Matangazo	2.97	3.12	3.27
Matukio na Ufadhili	3.70	4.20	5.10
Gharama za Bodi	2.14	2.25	2.36
Gharama za Kutunza Fedha	0.04	0.04	0.04
Jumla ya Uendeshaji na Matengenezo	390.68	416.32	448.19
Uchakavu	25.25	28.50	31.12
Faida ya Uwekezaji	70.45	65.45	63.92
Jumla ya Mahitaji ya Fedha	486.38	510.27	543.23
Ondoa: Mapato mengineyo	5.73	5.78	5.72
Mahitaji ya Fedha kwa Mauzo ya Maji	480.66	504.49	537.51
Uzalishaji wa Maji (Katika Mita za Ujazo)	614,880	614,880	614,880
Upotevu wa maji (%)	23	22	20
Maji yaliyouzwa (katika mita za ujazo)	467,309	479,606	491,904
Wastani wa Bei kwa Mita ya Ujazo)	**1,028.55**	**1,051.88**	**1,092.72**

Dodoma,
21st Aprili, 2020

NZINYANGWA E. MCHANY,
Mkurugenzi Mkuu